

CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO



NDAKI YA MISITU WANYAMAPORI NA UTALII

MKARATUSI

(*Eucalyptus spp.*)



Family: Myrtaceae



Kimetolewa na

Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii,  
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,

S. L. P 3009,

Chuo Kikuu,

MOROGORO TANZANIA

Tel. Gen. Line 255 023 2603511/4 Ext. 4601

E-mail: [forestry@suanet.ac.tz](mailto:forestry@suanet.ac.tz)




## MAELEZO YA JUMLA

Mikaratusi ni miti ya majani mapana. Mikaratusi mingine inakuwa miti mikubwa sana (ni kati ya miti mikubwa sana duniani) na mingine inakuwa midogo kama vichaka (hivyo kutumika kama uzio au mapambo).



Asili yake ni Australia, Papua New Guinea na Tasmania.

Ipo mikaratusi inayostawi kwenye sehemu ambazo ni nusu tropiki, Mediteranean, na nyingine tropiki.



## UKUZAJI

Katika sehemu nyingi hupandwa katika nafasi  $2.5 \times 2.5$  m mpaka  $3 \times 3$  m, kupata miti ya unene wa 15-20 cm inayotumika kama nguzo. Kupunguzia (thinning) huwa inaweza kufanya katika miaka ya 7, 11 na 15 hadi kufikia miaka 30 inapokuwa imekomaa kabisa kwa mbao.

## FAIDA ZA MIKARATUSI;

Mbao, dawa, kuni, mafuta ya mikaratusi (fuel), nguzo za umeme (E camaldulensis, E marginata), fanicha (E maculata, E globules), karatasi (E botryoides, E globules, E grandis), manukato(perfumes),



Mafuta ya Mkaratusi

Inasaidia uzalishaji wa asali, kukinga upepo, kupunguza mmomonyoko wa udongo, n.k. Ikitatwa inachipua haraka (coppicing). Hahitaji kupandwa upya hivyo kuleta mapato kwa muda mfupi.



- Mikaratusi ipandwe kwenye sehemu ambazo si vyanzo vya maji na sisizofaa kwa kilimo.
- Mikaratusi ni mwokozi wa misitu ukuaji wake wa haraka unaifanya kuwa mali asili yenyne mzunguko wa haraka, kwa kutoa kuni, mba, nguzo, mafuta nk. Hivyo kupunguza mzigo unaotokana na kuotesha maeneo makubwa ya miti mingine, na kungoja kwa muda mrefu kutoa faida kwa maana ya matumizi



- Sehemu nyingine duniani mikaratusi imekua chanzo kikubwa cha uchumi (economic boom), kwa kuwa ina wingi wa matumizi na pia inakua haraka.

